**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR – TAMISEMI).**

SHULE YA SEKONDARI NGASARO,

S.L.P. 113,

SHIRATI – RORYA.

01/12/2023.

KUMB. Na. NSS/JOIN/VOL.4/2023

MWANAFUNZI:………………………………………………

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA KUTWA SEKONDARI YA NGASARO KWA MWAKA 2024.**

Tafadahali rejea mada tajwa hapo juu. Napenda kukutaarifu kwamba, umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari ya Ngasaro kwa mwaka wa masomo 2024.

Shule ya sekondari Ngasaro inapatikana katika Mtaa wa Ngasaro – Shirati, mita chache kutoka barabara kuu ya kwenda Tarime, karibu na shule ya msingi Ngasaro. Unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe 08/01/2024 (siku ya kufungua shule). Mwisho wa kuripoti ni tarehe 08/02/2024. Unapaswa kuripoti shuleni ukiwa na mambo yafuatayo:-

1. **SARE ZA SHULE:**
   - ✓ Shati mbili nyeupe (Tomato) za mikono mifupi kwa wasichana na wavulana.
   - ✓ Tai moja rangi ya jani la mgomba (Idara ya jeshi) na moja rangi ya idara ya maji.
   - ✓ Suruali moja rangi ya jani la mgomba (Idara ya jeshi) na moja idara ya maji zenye mfuko mmoja nyuma. Upana wa chini (mguu) usipungue cm 17, isiwe modo wala mtindo wa piston.
   - ✓ Sketi moja rangi ya mgomba (Idara ya jeshi) na moja idara ya maji zenye rind box kubwa moja mbele na nyuma. Pembeni ndogondogo nne isiyobana iwe ndefu inayofika kwenye kisigino inchi 14 kwenda chini.
   - ✓ Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi jozi mbili kwa wavulana.
   - ✓ Viatu vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu wala kuchongoka mbele. Hii ni kwa wavulana na wasichana.
   - ✓ T-shirt moja dark gray yenye kola ya bendera ya taifa mikononi isiyo na muhuri au nembo.
   - ✓ Vifaa vya michezo: awe na viatu vya michezo jozi moja na soksi zake kwa wavulana na viatu vya raba na soksi zake kwa wasichana pamoja na track suit moja ya light blue yenye michirizi myeupe pembeni, kwa wote.

2. **VIFAA VYA KUJIFUNZIA:**
   - ✓ Counter book 10 za kuandikia nukuu (isiwe chini ya Quier 2)
   - ✓ Kamusi ya Kiingreza (English dictionary)
   - ✓ Kitabu cha **"Hawa the bus driver."**
   - ✓ Kalamu za wino na za mkaa kwa ajili ya kuandikia na kuchorea.
   - ✓ Mathematical set.
   - ✓ Bando moja ya karatasi (Ream) kwa ajili ya mitihani na mazoezi mbalimbali.

- ✓ Kwa wavulana waje na ndoo ndogo (Lita 10) na jembe.
- ✓ Kwa wasichana waje na ndoo na fyekeo ( slasher).
- ✓ File la kuhifadhia nyaraka zako za kitaaluma.

**3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE:**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Namba 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa sheria Namba 10 ya mwka 1995. Aidha kwa kuzingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu.

Hivyo, ukiwa mwanafunzi wa shule hii, unatakiwa kufuata maelekezo yafuatayo:-

i) Unapaswa kuripoti shuleni muda wa saa 12:45 asubuhi kila siku za masomo.
ii) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
iii) Kuheshimu viongozi, walimu na wafanyakazi wengine, wazazi, viranja, wanafunzi wenzio na jamii kwa ujumla.
iv) Kushiriki shughuli mbalimbali za shule, ikiwa ni pamoja na zile utakazopangiwa na walimu na viongozi wako.
v) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vi) Kuzingatia ratiba ya shule kama inavyoelekeza.
vii) Kutunza mali ya umma.
viii) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote uwapo shuleni.
ix) Kutokuwa na simu katika eneo la shule.
x) Kuongea / kuzungumza Kiingereza uwapo shuleni.

**MUHIMU:** Makosa yafuatayo yanaweza kukusababishia kufukuzwa au kusimamishwa shule mara moja.

i) Kuwa mja mzito au kupata mimba.
ii) Kutoa mimba.
iii) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
iv) Kukataa adhabu kwa makusudi.
v) Kudharau bendera ya Taifa.
vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, mirungi, kuberi n.k.
viii) Ubakaji.
ix) Uashereti na ushoga.
x) Wizi.
xi) Kupigana au kupiga.
xii) Kuwa na simu shuleni.

## HATI YA MAKUBALIANO

## KUKUBALIKUFUATA SHERIA NA UTARATIBU WA SHULE

Mimi ............................................................ nakubali nafasi ya kidato cha kwanza niliyopewa katika shule yako.

Nakubali kufuata sheria na utaribu wa shule hii na kuwa nitatii sheria zote zilizopo na zile zitakazowekwa kuwatii walimu wote na wafanyakazi kama walezi wangu.

Naahidi kuwa nitajielimisha kwa nguvu zangu na akili zangu zote kwa manufaa yangu binafsi na Taifa langu.

Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mtiifu na mwaminifu mbele ya raia wote popote nitakapokuwa. Natambua kuwa nikikiuka sheria na taratibu za shule pia ahadi yangu nitachukuliwa hatua kali.

Mimi .................................................. Mzazi/mlezi wa mwanafunzi huyu naahidi kuwa nitamhimiza mwanangu kufuata na kutii sheria za shule pia nitamtimizia mahitaji yote muhimu ya shule.

Jina la mwanfunzi: ............................................sahihi .................

Jina la mzazi/mlezi ......................................... Sahihi .................

Namba ya simu/Email .........................................................................

Kazi ya mzazi/mlezi .............................................................................

Jina mwenyekiti wa mtaa ................................ Sahihi .....................

Muhuri wa mwenyekiti wa mtaa

.........................................

**NATHIBITISHA**: Hakikisha unapo ripoti shule siku ya kwanza unafika na vitu vifuatavyo:-

(i) Medical exasmination form, ambayo imejazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali na si vinginevyo.

(ii) Kivuli cha chei cha kuzaliwa

(iii) Hati ya makubalino iliyojazwana kuongw muhuri.

Karibu sana

.....................

MAHUMA R.A

MKUU WA SHULE

**PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**NGASARO SECONDARY SCHOOL P.O.BOX 113, SHIRATI – RORYA**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by a medical officer in respect of all one (s) new entrants

Fula name: ………………………………………………………………………
Age: ……………………………………………………………………………
Blood count (red and white) ……………………………………………………
Stool examination: ………………………………………………………………
Urine analysis: …………………………………………………………………
Syphilis test: ……………………………………………………………………
T.B Test: ………………………………………………………………………
Ears: ……………………………………………………………………………
Spleen:…………………………………………………………………………
Abdomen (pregnancy) …………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION** e.g physical defects or impalement infections, chronic of family diseases ect.

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

From the results shown above I certify that above pupils is to pursue studies
Signature ………………………………………………………………………
Designation ……………………………………………………………………
Station ………………………………………Date: ……………………………

This from should be well complete and brought as the student comes to school for admission. It is very essential I accordance to students enrolments as it certifies physical fitness.